

102/3

KISWAHILI

KARATASI YA 3

KIDATO CHA NNE (4)

FASIHI

MACHI 2013

SAA:  $2\frac{1}{2}$

## MTIHANI WA MJARABU WILAYA YA BARINGO KASKAZINI - 2013

### Hati ya kuhitimu Kisomo cha Sekondari (K.C.S.E.) KIDATO CHA NNE

#### MAAGIZO

- *Jibu maswali manne pekee.*
- *Swali la kwanza ni la lazima.*
- *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki; yaani: riwaya, tamthilia, ushairi na hadithi fupi.*
- *Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.*

## **Swali la Lazima**

### **Sehemu ya A: Fasihi Simulizi**

1. (a) Kwa kutolea mifano eleza sifa bainifu za aina za maghani. (Alama 10)
- (b) Fafanua sifa za vitendawili. (Alama 5)
- (c) Ni nini dhima ya miviga. (Alama 5)

### **Sehemu ya B: Riwaya**

#### **Utengano - Said A. Mohamed**

#### **Jibu swali la 2 au la 3**

2. "... hakuweza kuzizua hisia zake, alilia taratibu kwanza, halafu sauti ilizi kuwa kubwa, akalia kwa kwikwi ..."
  - a) Weka dondo hili katika muktadha wake. (Alama 4)
  - b) Onyesha jinsi anayerejelewa anaendeleza maudhui ya mabadiliko. (Alama 8)
  - c) "Msiba wa kujitakia hauna kilio" thibitisha ukweli huu ukirejelea anayerejelewa kwenye dondo hili. (Alama 8)
3. Mbinu ya jazanda imefaulisha usanii wa mwandishi. Thibitisha. (Alama 20)

### **Sehemu ya C: Ushairi**

4. **Soma mashairi yafuatayo kisha ujibu maswali.**

#### **SHAIRI A**

Tunda la elimu zote, wasema wanazuoni  
Ni kwamba mtu apata kutambua manani  
Ndipo hadhi aipate, ukumbukwe duniani.

Elimu bila ukweli, haizidi asilani  
Giza na nuru muhali, katu havitangamani  
Uwongo uje kwa kweli, itue nuru moyoni.

Elimu ni kama mali, haichoshi kutamani  
Ni bora yashinda mali, tala la wanazuoni  
Elimu njema miali, iangazayo gizani.

Mtu hachomwi na mwiba, na viatu mguuni  
Ulimwengu una miba, tele tele majiani  
Elimu ukiishiba, u salama duniani.

Wafuna wasiosoma, watazikwa ardhini  
Hai ndio maulana, wapao maangani  
Elimu jambo adhima, aso nayo maskini

Toa wafu ujana, elimu ukitamani  
Na uwe mzee sana, kujua usijihini  
Elimu bahari pana, milele hauoni pwani.

Elimu ina malipo, utayalipwa mwishoni  
Pale vitafutapo, mbingu usitamani  
Mwanachumi afapo, mbingu huwa huzuni.

Haki ya kuhe shimiwa, ni yao wanachumi  
Wa wampongolewa, na ni taa duniani  
Kwezi wanapojuia, watoe bila kuhini.

Elimu bila amali, mti usio majani  
Haumtii kivuli, aukaliaye chini  
Inakuwa mushkeli wa kughuri insani

#### SHAIRI B

Inakera moyo  
Hii anga ambayo  
Huwasonya njiani  
Watukao mashambani  
Wa kusalimu kwa bashasha  
Wanaoshinda kivulini.

Chini ya mwembe  
Wa umma

Inakera moyo  
Hii sebule ambayo  
Huwahini mezani  
Wagotao nyundo kutwa  
Wa kukabidhi chakula  
Wanaostarehe daima

Chini ya paa  
La umma

#### Maswali

- a) Pendekenza kichwa kifaacho kwa shairi la A na B. (Alama 2)
- b) Haya mashairi ni ya aina gani? (Alama 2)

- FOR More Free KCSE past papers visit [www.FreeKCEPapers.com](http://www.FreeKCEPapers.com)
- c) Taja sifa zozote tatu za kishairi katika shairi B. (Alama 3)
  - d) Taja mbinu ya lugha iliyotumiwa;
    - i) Katika mshororo wa mwisho wa ubeti wa saba katika shairi la A. (Alama 1)
    - ii) Katika ubeti wa nne shairi la B. (Alama 1)
  - e) Fafanua kwa mukhtasari mandhui ya mashairi yote mawili. (Alama 4)
  - f) Andika ubeti wa mwisho wa shairi la A katika lugha tutumbi. (Alama 3)
  - g) Taja na uonyeshe jinsi idhini ya ushairi ilivyotumika katika shairi la A. (Alama 2)
  - h) Eleza maana ya maneno haya yalivyotumika katika shairi la A. (Alama 2)
    - i) Wameongolewa
    - ii) Wagotao

### **Sehemu ya D: Hadithi fupi**

**Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine**

**Ken Walibora na Said A. Mohamed**

**Jibu swali la 5 au la 6**

5. “Kama alivyoshinda nani yule ..... nunez?”
- a) Liweke dondo hili katika muktadha wake. (Alama 4)
  - b) Linganua sifa nne za msemaji na msemewa katika dondo hili. (Alama 8)
  - c) Kwa kurejelea hadithi nzima eleza hisia za utamaduni ulipitwa na wakati. (Alama 6)
  - d) Ni mbinu zipi za lugha zilizotumika katika dondo hili? (Alama 2)
6. Mwanamke katika diwani ya Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine amepewa nafasi finyu. Fafanua kwa kuzingatia hadithi zozote nne. (Alama 20)

### **Sehemu ya E: Tamthilia**

**Mstahiki Meya - Timothy M. Arege**

**Jibu swali la 7 au la 8**

7. “Mtu huvuna alichopanda. Ukipanda pojo huwezi kuvuna kunazi”
- a) Eleza muktadha wa dondo hili. (Alama 4)
  - b) “Ukipanda pojo huwezi kuvuna kunazi” ina maana gani kulingana na muktadha huu. (Alama 6)
  - c) Taja na ueleze matendo mengine manne ya kuonyesha kuwa walipanda pojo na kuvuna pojo si kunazi. (Alama 8)
  - d) Taja tamathali za usemi zilizotumiwa katika dondo hili. (Alama 2)
8. Suala la mawaidha mazuri na mabaya limeshughulikiwa tamthiliani. Onyesha jinsi Meya alivyoshauriwa vibaya na athari zake. (Alama 20)